JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI
MAMLAKA YA UDHIBITI WA
HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI
(EWURA)

# TAARIFA KWA UMMA

**(Imetolewa chini ya Kifungu cha 19 cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji, Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania)**

**T**aarifa inatolewa kwa umma kwamba Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imepokea maombi ya Leseni ya Muda ya Kuzalisha Umeme kutoka kwa kampuni ya Convivium Renewable Limited. EWURA inakaribisha maoni au pingamizi dhidi ya maombi hayo. Taarifa za mwombaji, mitambo na aina ya leseni iliyoombwa zimetolewa hapa chini:-

| **KIFUNGU** | **MAELEZO** |
|---|---|
| **Jina na anuani ya Mwombaji** | Convivium Renewable Limited,<br>S.L.P 123391,<br>Dar es Salaam. |
| **Mahali ulipo Mtambo** | Kijiji cha MWagalala, Kata ya Mabuki, Wilaya ya Misungwi District, Mkoani Mwanza. |
| **Taarifa za Wanahisa** | 1. Renergy Solar Tanzania I ApS, Marielundvej 20, 2730 Herlev, Denmark, **60%**<br>2. Convivium Investment Kenya Ltd, Nairobi, Kenya, **15%**<br>3. Mwangaza Solar Investment Ltd, Dar es Salaam, **15%**<br>4. Proin Limited, Dar es Salaam, Tanzania, **10%** |
| **Maelezo ya Mtambo** | Mtambo wa kuzalisha umeme wa Megawati (MW) kumi (10MW) kwa kutumia nishati ya jua. Umeme utakaozalishwa utauzwa kwa TANESCO kwaajili ya usambazwaji. |
| **Aina na Muda wa Leseni** | Leseni ya Muda Kuzalisha Umeme kwaajili ya kuuza kwa TANESCO kwa muda wa miaka mitatu (3) |

Mtu yeyote mwenye maoni au pingamizi kuhusu maombi haya awasilishe kwa maandishi ndani ya siku ishirini na moja (21) tangu siku ya kutolewa kwa tangazo hili. Nyaraka za maombi ya leseni zinaweza kuoneshwa kwa mtu atakayewasilisha maombi kwa maandishi.

Imetolewa na:-

**Mkurugenzi Mkuu**
06 Machi 2026